**TAMKO KWA UMMA**

**KULAANI TUKIO LA UTEKWAJI NA MAUAJI YA KIKATILI KWA MTOTO MWENYE UALBINO (ASIMWE NOVATH)- MULEBA KAGERA**

**Ndugu wanahabari,**

Kwa masikitiko makubwa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC) pamoja na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) tunalaani vikali tukio la utekwaji na mauaji ya kikatili kwa **Asimwe Novath (ambaye ni mtoto mwenye ualbino)** aliyekuwa na miaka miwili na miezi sita, mkazi wa kitongoji cha Mbale kijiji cha Bulamula kata ya Kamachumu wilaya ya Muleba mkoani Kagera. Tamko hili linakuja siku chache baada ya tamko la kukemea kutekwa kwa mtoto huyo na kutoa wito kwa mamlaka husika kupitia vyombo vyake vyote vya ulinzi na usalama kuhakikisha mtoto Asimwe Novati anapatika na wahusika wote wanafikishwa mbele ya sheria.

Itakumbukwa kwamba, mnano tarehe 30 mwezi Mei, 2024 kuripotiwa tukio la kutekwa kwa mtoto wa miaka miwili (2) mwenye ualbino aitwaye Asimwe Novati ililiofanywa na watu wasiyojulikana katika Kijiji cha Bulamula, Kitongoji cha Mbale, Kata na Tarafa ya Kamachumu wilayani Muleba mkoani Kagera siku ya tarehe 30 mwezi Mei, 2024. Iliripotiwa kuwa watu hao walimvamia kwa kumkaba mama wa mtoto huyo aliyejulikana kwa jina la Kebyera Richard, na kisha kumchukua na kukimbia na mtoto huyo kusikojulikana. Takribani siku kumi na nane (18), siku ya tarehe 17 Juni, 2024 iliripotiwa kupatikana kwa mwili wa mtoto huyo ukiwa umekatwa viungo vyake ikiwemo mikono, ulimi na macho.

Kwa mujibu wa taarifa kutoka kwa Katibu tawala wa Wilaya ya Muleba Ndugu Benjamini Mwakasyege, amesema kuwa mwili huo umekutwa umetelekezwa kwenye karavati yenye maji ya barabara ya Makongora, kijiji cha Malele.

Ukatili dhidi ya watu wenye ualibino unaweka taswira mbaya kwa nchi yetu na kuonyesha kuwa hakuna usalama kwa watu wake hususani watu wenye ualbino, tukio la kuuawa kwa mtoto Asimwe Novati ni tukio la kinyama, linalotweza utu wa mwanadamu na kurudisha upya taswira mbaya iliyotokea miaka michache dhidi ya ukatili wa watu wenye ualbino. Tukio limeendeleza kumbukumbu za matendo ya kikatili, tangu kunusurika kifo kwa mtoto mwenye ualbino aitwaye **Kazungu Julius mwenye umri wa miaka kumi (10)** mkazi wa Katoro mkoani Geita baada ya kuvamiwa na watu wasiyojulikana na kumkata mapanga sehemu mbalimbali za mwili wake hali iliyopelekea kuvuja damu nyingi.

**Ndugu wanahabari,**

Ni wazi kuwa mashambulizi dhidi ya watu wenye ualbino yamerudi kwa kasi katika kipindi hiki kuelekea uchaguzi hasa kwa watoto, itakumbukwa mwaka 2015 mkoani Rukwa kulitokea tukio la kushambuliwa kwa mtoto wa kiume aitwaye **Baraka Cosmas mwenye umri wa miaka sita (6)** akiwa amelala na mama yake mzazi ambapo watu wasiyojulikana walivamia nyumbani kwao na kumkata kiganja.

Tukio hili ni ukiukwaji wa wazi wa *Ibara ya 14 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 inabainisha ulinzi wa haki ya kuishi, Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Watu wenye Ulemavu, 2006, Tamko la Ulimwengu la Haki za Binadamu, Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu na Mikataba ya Kimataifa ya Haki za Binadamu pamoja na sheria za nchi ikiwemo Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura Namba 16 (Marejeo ya 2019).* THRDC na LHRC inalaani vikali vitendo hivi vya kikatili, kinyama na kihuni dhidi ya ndugu zetu wenye ualbino.

Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC) na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) kwa kipekee tunatoa pole na tunasimama na familia ya marehemu Asimwe Novath katika kipindi hiki kigumu cha msiba. Hakuna mtoto anayestahili kufanyiwa vitendo vya kikatili namna hii kwa sababu ya hali au mwonekano wake.

Masikitiko yetu makubwa ni namna mamlaka husika iilivyochukulia jambo hili, THRDC na LHRC hatujaridhishwa na mwitikio wa mamlaka husika ikiwemo kutoa taarifa kwa umma kujulisha jitihada zilizochukuliwa punde baada ya

taarifa ya kupotea kwa mtoto huyo, pia hakukuwa na taarifa yoyote kwa umma juu ya kuwatafuta watu waliofanya tukio hilo. Jambo hili linaongeza hofu kwa jamii ya watu wenye ualbino kuhusu usalama wao katika nchi yenye amani na sifa ya kulinda Haki za Binadamu.

Tukio hili la kinyama na kikatili dhidi ya mtoto huyu mwenye ualbino linapaswa kuikumbusha serikali na mamlaka zote husika kuhusu uhitaji mkubwa wa juhudi za pamoja za kukabiliana na unyanyasaji na ukatili dhidi ya watu wenye ualbino katika jamii zetu.

Siku ya tarehe 18 Juni, 2024 *(Jana)*, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, **Mhe. Samia Suluhu Hassan** katika Kongamano la Maendeleo ya Sekta ya Habari, alieleza masikitiko yake na kuumizwa sana na tukio la mauaji ya mtoto Asimwe Novath.

**Ndugu wanahabari,**

**Tunapenda kuikumbusha Serikali kuwa**, mapema mwaka huu, Kamati ya Umoja wa Mataifa ya Haki za Watu Wenye Ulemavu (CRPD) ilieleza masikitiko yake kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutokuwa tayari kufuatilia **maombi matatu yaliyowasilishwa** kwenye Kamati hiyo kuhusu ukataji viungo vya watu wenye ualbino na kutowajibika kwa Tanzania dhidi ya matukio hayo, Kamati hiyo ilisema kwamba, kushindwa kwa Tanzania kulaani na kuchunguza mashambulizi dhidi ya watu wenye ualbino kunaweza kuwa ni ukiukwaji mkubwa wa wajibu wake wa kuwalinda watu wenye ulemavu.

THRDC na LHRC tunatoa wito kama ifuatavyo;

1. Jeshi la polisi kufanya uchunguzi wa kina juu ya tukio hili na kuhakikisha kuwa wahusika wote, ikiwemo walioratibu utekelezaji, uuaji na watumiaji wa viungo vya watu hao na kuwafikisha kwenye vyombo vya sheria haraka iwezekanavyo.
2. Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Ajira, Vijana na Watu wenye Ulemavu) kuweka mikakati madhubuti ya kuwatambua na kusimamia ustawi watu wote wenye ualbino katika maeneo yote ya nchi.
3. Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutumia kipindi hiki cha Bunge la bajeti kujadili na kuweka fungu maalum ili kuimarisha mifumo ya ulinzi wa kwa watu wenye ualbino, hii ni katika ngazi zote kuanzia Kitongoji, Kijiji, Kata, Wilaya, Mkoa na Kifaifa ili kuhakikisha maisha ya

watu wenye ualbino yanalindwa na watu hao waendelee kufurahia maisha yao kama watu wengine katika jamii.

4. Jamii kuripoti watu wote wanaojihusisha na vitendo hivyo ili vyombo vya ulinzi na usalama kuchukua hatua za kipelelezi.
5. Jamii kuachana na imani potofu juu ya matumizi ya viungo vya watu wenye ualbino kwa kuhusisha na utajiri au kujipatia mamlaka katika ngazi mbalimbali.Tunawahimiza wanajamii wote kusimama pamoja kuibua na kutoa taarifa juu ya watu wote wanaofanya vitendo vya kikatili dhidi ya watu wenye ualbino kwa sababu ya imani za kishirikina.

Kwa sauti ya pamoja dhidi ya vitendo vya kikatili na unyanyasaji, tunasimama kwa umoja katika kukemea vitendo hivi na kusisitiza dhamira yetu ya kutetea haki za watu wote ikiwa ni pamoja na watu wenye ualbino nchini.

**Imetolewa leo tarehe 19 mwezi Juni 2024 na Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC) na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC).**

**Wakili Fulgence Massawe**

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji
Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC)

**Wakili Onesmo Olengurumwa**

Mratibu Taifa
Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu (THRDC)